# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

Januari 2019

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika". - Joseph Wresinski (1917-1988), founder of ATD Fourth World -

## Tahariri



Mpendwa Rafiki,

Tunayofuraha kubwa kuwapasha habari kuhusu maadhimisho ya Oktoba 17 ya mwaka huu hapa Tanzania na sehemu mbalimbali duniani. Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Pamoja Tujenge Dunia yenye kuheshimu Haki za Binadamu na Utu wa kilamoja".

Kulikuwa na kamati maalum ya kuandaa maadhimisho ya siku ya Kuutokomeza Umaskini Duniani, kamati ilikuwa na watu tofauti vijana, wazee na watu wazima. Tungependa tuwashirikishe jinsi maadhimisho ya mwaka huu yalivyo sherehekewa, wadau kotoka matabata tofauti tofauti kama vile mashirika, viongozi wa serikali za mitaa, manispaa, bima za afya, walimu na watu kutoka Rita pamoja na familia waliweza kushirikiana nasi.

Lengo lilikuwa ni kushirikishana kuhusu njia na jinsi wanavyopambana kila siku kuutokomeza umaskini uliokithiri na pia kushirikishana mawazo mapya kutoka kwa wadau tofauti tofauti ili kutusaidia kupiga hatua kwenda mbele na hiki ndicho wanachokitaka wana familia. Wadau waliweza pata fursa kusikia ni kwa jinsi gani watu wanaoishi katika umaskini uliokithi ni wanavyopambana kila siku kuutokomeza umaskini.


Ni watu wenye ujasiri mkubwa katika kupambana na umaskini na kuutokomeza, pia tukiungana na kushirikiana kwa pamoja itatupa njia /nafasi ya kujifunza sisi kwa sisi na kufikia malengo ya kuutokomeza umaskini.

Hii ni siku ya wadau wanaoishi katika umaskini uliokithiri na marafiki zao kujieleza na kupaza sauti zao kwa pamoja ili zisikike duniani kote kwa kusoma shuhuda zinanoelezea maisha yao na juhudi wanazozifanya katika kupambana na umaskini na kwa pamoja kutafuta njia bora ya kutokomeza.

Kwenye kurasa inayofuta utapata kusoma shuhuda zao.

Asante.

Salma Moshi
ATD Fourth World Tanzania



# "Wote ni kama mwili mmoja".

Siku ya Oktoba kumi na saba (17) ilikuwa ni fulsa kwa kila mmoja kuelezea namna gani anapambana dhidi ya Umaskini.

Watu wa tatu wanaofanya kazi ya kugonga mawe walitoa shuhuda juu ya changamoto zote wanazokabiliana nazo katika kazi yao:

Bwana Yohana alielezea zaidi namna watu wanavyoishi katika kazi. Ashura Said anasema, Kama una afya nzuri kugonga mawe ni kazi inayoweza kufanywa na kila mtu. (pitia ushuhuda wake kwenye ukurasa wa nyuma). Ndio maana wanaofanya kazi hii ni watu wengi walio na Elimu ndogo .

Kwa upande mwingine, kazi hii inahitaji kujitoa zaidi, mazingira yake ni hatarishi: Miongoni mwa ajali au madhara yanayoweza kujitokeza ni wakati unapotega baruti ili kulipua mawe makubwa, pia huambatana na magonjwa.



Kugonga mawe ni kazi inayoweza kukuletea magonjwa. Siku nzima kukaa chini ya jua, wakati mwingine changamoto ni watoto.

Wanawake huwa na magonjwa maalum kutokana na jinsia zao, kubeba mawe mara kwa mara hupelekea kuharibika kwa mimba.

Changamoto kama hizi za afya hujitokeza kutokana na ile hali ya kuwa watu hawana dhana za kujikinga. Kutokana na kukabiliana na changamoto hizi, watu wanaogonga mawe wameweza kuanzisha umoja wao, kama inavyoelezewa na Mr Yohana, " wote ni kama mwili Mmoja".

Shukrani kwa umoja huu ambao huweza kusaidiana kwa kupelekana hospitali, inatia moyo kuona kwamba kila mmoja hufanya jitihada kwa kupeana ushauri au kusaidiana kipesa pale inapobidi, Kipato ni kidogo sana. Mr Ash. "Kwa siku nzima baada ya kazi unaweza kupata elfu mbili (2000) mpaka elfu tano (5000)". Watu wanaofanya kazi hii wanawahimiza wengine kuungana nao katika kupambana na umaskini.

Wawakilishi kutoka mashirika ya IWAPOA na TASAO walielezea malengo na matazamio yao juu ya namna gani kwa pamoja wanaweza kufikiria na wagonga mawe ili kufanya kazi kwa pamoja siku za mbeleni.











## Ujumbe kutoka Tanzania (shuhuda ya Salehe Seif, voluntee wa ATD na Asha Athumani (mwenye uzoefu wa umaskini) katika hotuba ya Umoja wa Mataifa - New York

Nilivyokataliwa kupewa visa ya kwenda New York, niligundua kwamba watu wanaoishi katika umaskini ulikithiri mara nyingi ufedheheshwa na awaheshimiwi. Nilihisi haki zangu zemevurugwa, na kwamba sina fursa sawa ya kusafiri na kuwa sehemu ya dunia. Waliniambi kwamba hawawezi nipa visa kwa sababu hawakuniamini kama ningeweza rudi nyumbani baada ya maadhimisho ya tukio la tarehe 17 Oktoba. Nilisikitishwa sana; niliamini ningewashirikisha maarifa yangu na uzoefu wangu na pia kujifunza kutoka kwa wengine. Nilikataliwa visa kwa sababu thamani ya utu wangu haukuthaminiwa.

Maarifa na uzoefu wa watu wanaoishi katika umaskini hautiliwi maanani katika jamii na katika taasisi. Ni kama vile wako jela katika uzio, hakuna mtu anaewaamini , hawana nafasi au fursa ya kujieleza wenyewe moja kwa moja. Watu wanaoishi katika lindi la umasikini wanakutana pamoja wao kwa wao; sehemu pekee wanapokosekana ni katika ngazi ya watunga sera. Watunga sera wanapopanga shughuli au mipango ya maendeleo kuhusu walioachwa nyuma hawajumuishwi. Lakini wao ndio wanaoishi katika umaskini, na wao wanakitu cha kuchangia na mapendekezo kuhusu ni nini kinachofanya maisha yao kuwa katika ubora.

Haki za binadamu na Utu wa kila mmoja ukitiliwa maanani dunia itakuwa na Amani endelevu na upendo. Nilikuwa mmoja kati ya wanafunzi wanaofanya vizuri pamoja na umaskini wangu na kuangaika. Ingawaje, mama yangu alinishauri nifeli mtihani wangu wa Taifa kumaliza shule ya msingi. Alikuwa na wasiwasi na khofu kuhusu gharama za shule ya secondary kwani alikuwa pekeyake kwa sababu ya upweke wa umaskini uliokithiri tuliokuwa tunakabiliana nao. Kipindi hiko iwapo mtoto atafauli mtihani wake wa taifa na wazazi wasipompleka mtoto shule ya sekondari wangeweza pelekwa jela. Na vilevile ni chanzo cha aibu kwa wazazi pale mtoto wao anapofaulu mtihani na kushindwa kuwapeleka watoto katika shule za sekondari.

Je, mama Asha alikuwa na chaguzi nyingine? Unanweza ona kwamba ni jinsi gani ufukara pia unavyokulazimisha kuchagua kitu ambacho unajua ni kitu usichokitaka wewe mwenyewe na kwa familia yako

Watu wanaoishi katika umaskini si ombaomba, si wenye kulalamika, si kimbelembele wenye kusema nahitaji msaada, maranyingi hufanya kazi kwa bidi, wanafanya kila liwezekanalo kuuficha umaskini wao. Wanahakikisha wanavaa nguo safi ni njia moja wapo ya kujilinda Utu wao. Hivo wanawezaje kufikiwa na mifumo ya ulinzi? Haitoshi kuuliza kupitia utafiti kama nyumba yako ni ya nyasi au bati, kufahamu nani maskini wa kutupwa katika jamii. Watu wanaoishi katika umaskini wenyewe wanajua na wanaweza kusema nani anastahiki kusaidiwa na maswali gani ni sahihi yakuulizwa watu wanaoishi katika umaskini. Tunasaidiana sisi kwa sisi ispokuwa hatuna nyenzo za kufanya hivyo.

Ili tufanikishe malengo yetu ya kutokomeza umaskini uliokithiri, ushirikishwaji ni muhimu na watu wenye uzoefu wa umaskini uliokithiri moja kwa moja ni wadau muhimu. Wanamawazo mazuri, maoni na mapendekezo katika kufikia malengo. Maarifa yao yanapounganishwa na wanazuoni na watalamu, matokeo yanakuwa yamekamilika na hakuna mtu atakaeachwa nyuma.

Ushirikishwaji inaruhusu wananchi wote au jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo katika jamii au nchi zao. Watu wanaposhirikishwa kila mmoja ufahamu kinachoendelea katika jamii na watu wanakuwa na hisia ya kujivunia. Kwa mfano, katika ATD Dunia ya Nne Tanzania ulifanywa utafiti shirikishi wa mafanikio juu ya elimu kwa wote, watu wenye uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini uliokithiri. Shule zote zilizojihusisha katika mradi huu zimekuwa na matoke chanya. Kipindi cha nyuma shule hizo hazikukuwa na mawasiliano mazuri kati ya walimu, wazazi na wanafunzi, lakini kwa sasa mahusiano mzuri yapo. Na hufanya watoto wapende kusoma. Utafiti unapowashirikisha wadau wote; kama vile walimu, wazazi, mamlaka za mitaa, maafisa elimu na mwisho wake tumepata mafanikio. Ushirikishwaji unajenga ujasiri, hali ya kujiamini na maarifa, na upanua mawazo na pia uwezo wa kufanya uamuzi sahihi. Kutoachwa mtu nyuma, tunabidi tuwajumuishe wote katika kila hatua ya kubuni, utekelezaji na tathimini ya sera.



# Ushuhuda wa Ashura, Mgonga mawe maeneo ya "Cambodia Quarry" Boko

Jina langu ni Ashura Onesmo, ni Mama wa watoto watano (5), ni mgonga mawe maeneo ya "Cambodia". Chanzo cha Umaskini wangu ni mgogoro wa kifamilia kati ya wazazi wangu Baba na Mama. Mama yangu alikuwa ni mtu mwenye kipato kidogo sana kupitia shughuli zake ndogondogo. Lakini niliweza kumaliza Elimu yangu ya msingi darasa la saba (7). Sikuweza kumudu kuendelea na Elimu ya juu zaidi. Nafikiri kama ningekuwa na elimu nzuri ningeweza kupata kazi nzuri na kupambana na Umaskini,

Kwa sisi wakina Mama, Namna ya Kupambana na Umaskini ni Kuendelea Kugonga Mawe tu. Ni aina ya kazi ambayo haihitaji kuwekeza zaidi ya nguvu zetu. Ingawa kazi ya kugonga mawe ni ngumu na ni ya hatari, bado tunaendelea na kazi hii sababu hatuna kitu kingine mbadala cha kufanya.

Kawaida huwa ninaamka saa kumi (10) ya alfajiri, nina tayarisha juisi kwa ajili ya kuuza na kuandaa chakula cha mchana kabisa kabla ya kutoka kwenda kugonga mawe. Huwa nina wasili sehemu ya kugonga mawe saa kumi na mbili (12) Asubuhi bila ya kukawia huanza kugonga mawe. Ifikapo saa tisa (9) alasiri huanza kuyapima mawe niliyoyagonga kwenye ndoo. Kwa siku nzima ninaweza kujaza ndoo saba (7) mpaka ishirini (20) ambazo huniwezesha kupata shilingi elfu mbili (2000) mpaka elfu tano (5000). Ni kiasi cha pesa ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji ya familia lakini hakuna njia nyingine zaidi ya kuendelea kugonga mawe. Hatupaswi kukata tamaa huku tukiamini ipo siku mambo yatabadilika.

Kugonga mawe ni kazi ambayo inaweza kufanywa na kila mtu kwasababu haihitaji mtaji wowote zaidi ya nguvu kazi yako, hata hivyo ni kazi ya hatari sana, kama vile kupata Tibii kwasababu ya vumbi, kufanya kazi chini ya jua kali siku nzima bila ya kuwa na mlo wa uhakika, kwa sisi wanawake matatizo makubwa ni pindi pale tunapobeba mawe yenye uzito mkubwa hupelekea madhara ya kutoka kwa mimba hasa kwa wakina mama ambao ni wajawazito.

Changamoto za umaskini ni nyingi. Watoto wetu wadogo hulazimika kuambatana nasi kila siku na hujikuta wakikulia kwenye mazingira ya kugongea mawe. Taratibu huanza kugonga mawe wakiwa na umri mdogo na hupata kiasi kidogo cha pesa. Hali hii hupelekea baadhi ya watoto kutopenda tena shule kwa sababu ya kuendelea kupata pesa.

Kwa niaba ya wakina Mama ningependa kusema ahsanteni sana, Mungu aendelee kuwabariki.



ATD Dunia ya Nne - SLP 61786 - Dar es Salaam
Namba ya Ofisi: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
Kiswahili website: https://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/
Ukurasa wa Facebook: https://www.facebook.com/atd.duniayanne